


# Mabadiliko ya sera ya kujiandikisha

## Maelezo kwa familia

## Kwa nini kuchagua elimu ya umma?

Mfumo wa elimu ya umma ya NSW hutoa wanafunzi wote na elimu nzuri sana, ukitayarisha watoto wa sasa kufanikia na kupata jamii nzuri zaidi kwa baadaye. Pamoja na utoaji wa elimu ya ubora wa juu, yenye kiujumla na fursa zisizo na kifani za mitaala shirikishi katika Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati, sanaa, michezo na kwingineko, shule zetu mbalimbali za umma zinazojumuisha kila mwanafunzi zinasaidia kila mwanafunzi kufikia uwezo wake kamili.

## Sera ya uandikishaji ni nini?

Sera ya kujiandikisha husaidia shule kutimiza wajibu wao chini ya Sheria ya Elimu (Education Act 1990), kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaweza kupata shule zao za umma. Sera hiyo pia hutoa maelezo mazuri kwa wafanyakazi na jumuiya kuhusu jinsi uandikishaji unavyoshughulikiwa katika shule za umma za NSW.

## Kwa nini sera inabadilika?

Idara ya elimu ya NSW ilishauriwa na washirika wa elimu, vikundi vya jamii na timu za uongozi wa shule juu ya sera ya kujiandikisha wa kisasa. Tulipokea maoni muhimu kuhusu umuhimu wa kushughulikia vizuizi ambavyo familia hukutana navyo wakati wa kujaribu kujiandikisha katika shule za umma za NSW. Sera iliyosasishwa ya uandikishaji inashughulikia vizuizi hivi na inapatana na dhamira ya idara ya kujenga na kudumisha mfumo wa usawa na kufikiwa wa shule za umma.

## Mabadiliko ni nini?

Mabadiliko yafuatayo yatatumika kwa uandikishaji wote unaoanza katika Kipindi cha 1 cha 2025.

### Wakazi wa muda

Wanafunzi wote walio na viza ya ukaji wa muda wataweza sasa kujiandikisha katika shule yao ya karibu, kulingana na anwani yao ya mkazi.

Ada za kujiandikisha zitafutwa kwa familia ambazo zinamiliki viza za Uhaba wa Ujuzi wa Muda (daraja la 482), yaani wale wanaoishi nje ya Sydney na Wollongong kubwa.

### Vigezo vilivyosasishwa vya uandikishaji usio wa karibu

Shule za umma za NSW zina maeneo maalum ya karibu ya kujiandikisha. Maeneo yaliyotengwa ya kuandikisha huamuliwa na idara. Shule hizi huhakikisha kuwa kuna nafasi za kutosha kwa wanafunzi wanaoishi katika eneo lao la kujiandikisha. Unaweza kutuma maombi ya kumwandikisha mtoto wako nje ya eneo ulilochaguliwa kama 'uandikishaji usio wa karibu', ikiwa nafasi zinapatikana.

Vigezo vilivyosasishwa vinaweka kipaumbele uandikishaji usio wa karibu kwa ndugu na dada wa wanafunzi waliojiandikishwa sasa, na huku kipaumbele kikipewa ndugu na dada wa wanafunzi waliojiandikisha katika madarasa ya usaidizi katika shule za kawaida zinazostahiki.

Chini ya vigezo vilivyosasishwa, shule zinaweza sasa kuzingatia uandikishaji usio wa karibui kwa watoto wa wafanyakazi wa shule.



NSW GOVERNMENT

## Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

### Je, mabadiliko hayo yanatumika kwa mtoto wangu?

Mabadiliko kwa uandikishaji katika shule za umma za NSW yanahusiana nawe ikiwa:

- mtoto wako ana umri wa kwenda shuleni na ana viza ya mkazi ya muda, au
- mtoto wako ana umri wa kwenda shuleni na ana mdogo au mkubwa aliyeandikishwa katika shule tofauti ya umma ya NSW na ungependa wasome shule moja. Uwezo wa shule kukubali uandikishaji wa mtoto wako unategemea uwezo wake na vigezo vya kustahiki.
- wewe ni mfanyakazi wa shule ya umma ya NSW nje ya eneo la uandikishaji la mtoto wako. Uwezo wa shule kukubali uandikishaji wa mtoto wako unategemea uwezo wake na vigezo vya kustahiki.

### Je, kila shule itahitajika kutekeleza mabadiliko haya?

Shule zote zinahitajiwa kutuma mabadiliko hayo kwa wanafunzi wenye viza za ukaaji wa muda.

Shule nyingi, kulingana na uwezo wao, zinahitajika kutumia mabadiliko ya uandikishaji usio wa ndani kwa wanafunzi wanaojiandikisha kwa Kipindi cha 1, 2025.

Mabadiliko ya sera ya kujiandikisha kwa wanafunzi wakazi wa muda na wanafunzi wasio wa karibu hayataathiri mahitaji ya kustahiki kwa mipangilio au miradi ya kitaalamu. Shule zenye vigezo vya kustahiki zikijumuisha shule zinazochaguliwa kabisa, shule za madhumuni maalum, (schools for specific purposes (SSPs)), shule za elimu ya mbali, na shule zenye madarasa au miradi yenye mahitaji fulani ya kustahiki, (kwa mfano, madarasa ya fursa, michezo ya kitaalamu na/au masomo ya sanaa ya kuona) zitaendelea kufuata mchakato wao wa kujiandikisha wa sasa.

Shule za watu wa jinsia moja lazima zitumie mabadiliko hayo mradi tu mtoto anayejiandikisha anaridhi mahitaji ya shule ya kustahiki jinsia hiyo. Wasiliana na shule husika ili kuuliza jinsi mabadiliko haya yanatumika.

### Ikiwa mtoto wangu ni ndugu au dada wa mwanafunzi aliyeandikishwa kwa sasa, je, ombi lake la kujiandikisha lisilo la ndani litakubaliwa kiotomatiki?

Mabadiliko haya hayahakikishi kuandikishwa kwa mtoto wako katika shule ya umma isiyo ya karibu kama ndugu na dada yake. Shule zitatanguliza uandikishaji usio wa karibu kwa ndugu na dada wa wanafunzi walioandikishwa kwa sasa inapowezekana, lakini kukubaliwa kwa ombi lao kunaweza kutegemea uwezo wa shule. Wasiliana na shule husika kwa habari zaidi.

### Je, hii inamaanisha kuwa ni ndugu na dada pekee ndiyo watakubaliwa kuandikishwa kama watu wasio wa ndani kuanzia sasa?

Hapana, unaweza bado kutuma ombi kuandikisha mtoto wako katika shule yoyote ya umma ikiwa mtoto anastahiki kuhudhuria shule ile na shule inaweza kumudu mtoto. Shule sasa lazima ziweke kipaumbele na kuzingatia maombi kulingana na vigezo vilivyosasishwa vya uandikishaji usio wa eneo lako (pamoja na vigezo vinavyohusiana na mahitaji ya ustawi wa wanafunzi), ambavyo vinawapa kipaumbele ndugu na dada wa wanafunzi walioandikishwa kwa sasa na kuzingatia watoto wa wafanyakazi wa shule.

### Je, ujiandikishaji usio wa karibu kwa watoto wa wafanyakazi wa shule utakubaliwa kiotomatiki?

Hapana. Shule itaweka kipaumbele maombi yasiyo ya karibu kwa ndugu na dada wa wanafunzi walioandikishwa kwa sasa, na kisha inaweza kuzingatia uandikishaji usio wa karibu kwa watoto wa wafanyakazi wa shule. Ikiwa wewe ni mfanyakazi wa shule, kukubalika kwa mtoto wako kunaweza kutegemea uwezo wa shule. Vigezo vilivyosasishwa vya kujiandikisha kwa wasio wa eneo lako havitaathiri haki ya mtoto wako ya kujiandikisha katika shule yake ya karibu.

## Kujiandikisha kwa wanafunzi wenye viza ya mkazi ya muda

**Mtoto wangu ana viza ya mkazi ya muda. Hapo awali nilituma maombi ya kumwandikisha katika shule yao ya karibu lakini ombi lilikataliwa. Je ninaweza kutuma tena ombi la kujiandikisha la mtoto wangu?**

Unaweza kutuma tena ombi lako la kuandikisha ikiwa mtoto wako ana viza ya mkazi ya muda na ombi lililopita kwa shule yako ya karibu lilikataliwa. Tafadhali fuata hatua zilizoelezwa katika sehemu ya hapa chini “Je, nifanyaje kubadilisha mahali ambapo nilipomwandikisha mtoto wangu kwa 2025?”

**Mtoto wangu ana viza ya mkazi ya muda na nimemwandikisha mtoto wangu katika shule kwa 2025. Je ninaweza kubadilisha mahali ambapo nimemwandikisha mtoto wangu?**

Ikiwa mtoto wako ana viza ya mkazi ya muda na tayari ameandikishwa katika shule kwa 2025, unaweza kuomba kubadilisha shule ambapo ameandikishwa kwa sasa. Tafadhali fuata hatua zinazoelezwa katika sehemu ya hapa chili “Je, nitabadilishaje mahali ambapo nimemwandikisha mtoto wangu kwa 2025?”

**Je, nitabadilishaje mahali ambapo nimemwandikisha mtoto wangu kwa 2025?**

Wazazi au walezi wa wanafunzi wenye viza ya mkazi ya muda wanahitaji kufuata hatua hizi ili kubadilisha uandikishaji wake kwa shule yao ya karibu.

1. Wasiliana na timu ya Mradi wa Wakazi wa Muda kwa simu kupigia simu kwa 1300 300 229 (chaguo la 1) au kwa email kwenye tempvisa@det.nsw.edu.au ili kuomba kubadilisha shule kwa mtoto wako. Utafahamishwa na timu ya Wakazi wa Muda mara baada ya uhamisho wa shule kwa mtoto wako kukamilika
2. Wasiliana na shule yako ya karibu kumwandikisha mtoto wako. Shule itakutolea na fomu ya ombi ya karatasi utakayohitaji kujaza ili kuandikisha. Pata habari za mawasiliano za shule yako ya karibu kwenye education.nsw.gov.au/find-a-public-school

**Mtoto wangu ni mkazi wa muda kwenye viza badala ya viza ya 482. Je, nahitaji kulipa ada za kujiandikisha?**

Ada ya ombi la mkazi la muda na ada ya kusoma ili kujiandikisha shule ya serikali huhesabiwa kwa kutumia daraja dogo la viza linaloshikilwa na mwanafunzi. Kwa habari za kina kuhusu ada zinazotumika kwa daraja dogo la viza yako, tafadhali tembelea tovuti ya DE International: deinternational.nsw.edu.au/study-options/study-programs/temporary-residents. Ikiwa bado huna hakika kama msamaha wa ada tunatumika kwako, unaweza kuwasiliana na timu ya Mradi wa Wakazi wa Muda kwenye tempvisa@det.nsw.edu.au

## Uandikishaji wa ndugu na dada wasio wanafunzi wa karibu

**Nilituma ombi kumwandikisha mtoto wangu katika shule ambayo ndugu yake anahudhuria lakini ombi lake lilikataliwa. Je, ninaweza kutuma tena ombi la uandikishaji wa mtoto wangu?**

Ikiwa umeomba kumwandikisha mtoto wako katika shule ya ndugu yake isiyo karibu na ombi limekataliwa, tafadhali fuata hatua zinazoelezwa katika sehemu hapa chini "Je, nitabadilishaje mahali ambapo nimemwandikisha mtoto wangu kwa 2025? kuwasilsha upya.

**Nilimwandikisha mtoto wangu katika shule kwa 2025, lakini ndugu yake ameandikishwa katika shule tofauti isiyo ya karibu. Je ninaweza kuomba kubadilisha shule ambapo ameandikishwa?**

Ikiwa unagetaka kubadilisha shule ambayo mtoto wako ameandikishwa kwa 2025 kuwa shule ile ile isiyo ya karibu ambayo ndugu yake anahudhuria kwa sasa, tafadhali fuata hatua zilizoelezwa katika sehemu ya hapa chini "Nitabadilishaje mahali ambapo nimemwandikisha mtoto wangu kwa 2025?" kuwasilisha upya.

**Je, nitabadilishaje mahali ambapo nimemwandikisha mtoto wangu kwa 2025?**

Wazazi au walezi ambao wangependa kumwandikisha mtoto wao katika shule ile ile isiyo karibu kama ndugu zao wanahitaji kufuata hatua hizo ili kubadilisha uandikishaji wao:

### Maombi ya kujiandikisha mtandaoni

1. Nenda kwa tovuti ya shule unayotaka kutuma ombi la kujiandikisha, kisha bofya kwenye uandikishaji katika chaguzi za menyu.
2. Kwenye ukurasa wa kuandikisha, chini ya kichwa cha jinsi ya kujiandikisha bofya kwenye kiungo kuelekea ombi la kujiandikisha mtandaoni.
3. Mara umetuma ombi lako la kujiandikisha, shule inaweza kukutolea ofa ambayo utahitaji kukubali ndani ya siku 14.
4. Ikiwa ombi lako linakubaliwa, wasiliana na shule ambayo mtoto wako aliandikishwa wakati iliyopita kwa 2025 ili kuondoa uandikishaji ule.

### Maombi ya fomu ya karatasi

1. Wasiliana na shule ya ndugu wa mtoto wako ili kujua kama inaweza kuchukua mtoto wako.
2. Iwapo shule inaweza kuchukua mtoto wako, kamilisha fomu mpya ya ombi ya karatasi, ambayo shule inaweza kutoa.
3. Mara umetuma ombi lako la kujiandikisha, shule inaweza kukutolea ofa ambayo utahitaji kukubali ndani ya siku 14.
4. Ikiwa ombi lako linakubaliwa, wasiliana na shule ambayo mtoto wako aliandikishwa wakati iliyopita kwa 2025 ili kuondoa uandikishaji ule.

**Nimetuma Onyesho la Nia (Expression of Interest (EOI)) kwa mpito wa Mwaka wa 6 kwenda 7 katika 2025. Je ninaweza kubadilisha mahali ambapo nimemwandikisha mtoto wangu?**

EOI kwa mpito wa Mwaka wa 6 kwenda 7 imefungwa kwa hiyvo wazazi na walezi hawawezi tena kufanya mabadiliko kwa orodha ya upendeleo wa shule kwa 2025.

Ikiwa unagetaka kubadilisha shule ambayo mtoto wako ameandikishwa kwa 2025 kuwa shule ile ile isiyo ya karibu ambayo ndugu yake anahudhuria kwa sasa, unapaswa kufuata hatua zifuatazo:

### Maombi ya kujiandikisha mtandaoni

1. Nenda kwa tovuti ya shule unayotaka kutuma ombi la kujiandikisha, kisha bofya kwenye jinsi ya kujiandikisha katika chaguzi za menyu.
2. Kwenye ukurasa wa kuandikisha, chini ya kichwa cha jinsi ya kuandikisha bofya kwenye kiungo kuelekea ombi la kujiandikisha mtandaoni.
3. Mara umetumwa ombi lako kujiandikisha, shule inaweza kutoa ofa ambayo utahitaji kukubali ndani ya siku 14.
4. Ikiwa ombi lako linakubaliwa, wasiliana na shule ambayo mtoto wako aliandikishwa wakati iliyopita kwa 2025 ili kuondoa uandikishaji ule.

### Maombi ya fomu ya karatasi

1. Wasiliana na shule ya ndugu wa mtoto wako ili kujua kama inaweza kuchukua mtoto wako. Pata habari ya mawasiliano ya shule kwenye: education.nsw.gov.au/find-a-public-school.
2. Iwapo shule inaweza kuchukua mtoto wako, kamilisha fomu mpya ya ombi ya karatasi, ambayo shule inaweza kutoa.
3. Mara umetuma ombi lako la karatasi la kujiandikisha, shule inaweza kukutolea ofa ambayo utahitaji kukubali ndani ya siku 14 au haraka iwezekanavyo.
4. Ikiwa ombi lako linakubaliwa na umeshakubali ofa yako ya EOI, wasiliana na shule ambayo mtoto wako tafadhali wasiliana na shule moja kwa moja ili kuondoa uandikishaji ule.

## Uandikishaji wa watoto wasio wa karibu wa wafanyakazi wa shule

**Nilituma ombi kumwandikisha mtoto wangu katika shule ninayofanya kazi, lakini ombi lake lilikataliwa. Je, ninaweza kutuma tena ombi la uandikishaji wa mtoto wangu?**

Iwapo umetuma ombi la kujiandikisha mtoto wako katika shule unayofanya kazi na ombi lile limekataliwa, unaweza kutuma tena. Kufanya hivi, tafadhali fuata hatua zinazoelezwa katika sehemu hapa juu chini ya "Je, nitabadilishaje mahali ambapo nimemwandikisha mtoto wangu kwa 2025?".

### Je, naweza kupata habari zaidi wapi?

**Kwa maswali ya uandikishaji, ongea na shule unayopendelea. Pata habari za mawasiliano za shule yako kwenye: education.nsw.gov.au/find-a-public-school**

**Kwa habari zaidi juu ya jinsi ya kujiandikisha katika shule ya serikali ya NSW: education.nsw.gov.au/enrolment**

**Kwa habari zaidi juu ya jinsi ya kujiandikisha katika shule ya serikali ya NSW kama Mkazi wa Muda: https://www.deinternational.nsw.edu.au/**

**Kwa maswali ya kijumla ya uandikishaji, wasiliana na ofisi kuu ya Idara ya Elimu: 1300 679 332**

**Huduma ya Wakalimani wa Simu**

Iwapo unahitaji mkalimani kukusaidia kuwasiliana na shule au Idara ya Elimu, tafadhali piga simu kwa Huduma ya Wakalimani wa Simu kwa 13 14 50 na omba kupata mkalimani wa lugha yako. Mwambie mpigaji simu nambari ile ya simu unayotaka kupiga na mpigaji simu atapata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia na mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii.